

SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi



Toleo Na. 010

Jarida la kila miezi mitatu

Machi - Juni, 2012


Makanisa Yachomwa Moto, Viongozi wa UAMSHO Mahkamani

JUMLA ya Makanisa matatu yalichomwa moto na mali za wamiliki mbali mbali katika Manispaa ya Zanzibar zimeharibiwa kufuatia ghasia za siasa zinazohusishwa na mfumo wa Muungano wa Tanzania.

Ghasia za siasa zinazohusu mfumo na uendeshaji wa Muungano wa Tanzania ulioasisiwa Aprili 26, 1964, zilitokea katika Mkoa wa Mjini Magharibi baina ya Mei 26-28, 2012 na inasadikiwa ziliongozwa na Jumuiya ya Uamsho na Mihadhara ya Kiislamu (JUMIKI).

Ghasia hizo zilizuka usiku wa Mei 26, 2012 baada ya kiongozi mmoja wa JUMIKI kukamatwa na Polisi na kufikishwa Kituo

Inaendelea Uk. 3



Kanisa la Assemblies of God lililopo Kariakoo, Unguja ambalo ni moja kati ya makanisa yaliyochomwa moto kutokana na fujo zilizodaiba kusababishwa na Jumuiya ya UAMSHO, Zanzibar.

Mtoto Mchanga Akatwa Pua Pemba

MTOTO mchanga wa mwezi mmoja Arafa Haji Silima amekatwa pua katika mazingira ya kutatanisha na kufariki dunia katika kijiji cha Mtipweke, Shehia ya Wesha, Wilaya ya Chake Chake, Mkoa wa Kusini Pemba.

Mama wa kichanga huyo, Bibi Pili Bakari Hilali alisema kwamba mtoto wake alikatwa pua saa nne za asubuhi Mei 15, 2012. Kichanga huyo alizaliwa April 12, 2012.

Alisema kwamba mtoto huyo alizaliwa pacha na mwenziwe wa kiume ambaye walikuwa wamelazwa pamoja siku ya tukio.

"Nilisikia kilio si cha kawaida. Nilipokwenda ndani nikamuona mtoto wangu amekatwa pua na nilimchukua kumpeleka Hospital ya Chake Chake na kufariki" alisema bi Pili huku akitokwa na machozi.

Msaidizi wa Sheria wa Jimbo la Chake



Sehemu ya jengo la Hospitali ya Chake Chake, Pemba alipopelekwa mtoto mchanga aliyekatwa pua na kufariki.

Chake, Bibi Riziki Hamad Ali aliyemhoji mama mzazi alisema hakuonekana mtu aliyemkata pua kichanga hicho.

Lakini alisema mtu mmoja anayetuhumiwa kumkata pua kichanga huyo ameripotiwa Kituo cha Polisi Chake Chake. Inasemekana imani za kishirikina zinahusishwa na tukio hilo.

Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar kinalaani kukatishwa haki ya kuishi na ukatili dhidi ya mtoto huyu. Kituo kinasisitiza Sheria ichukue mkondo wake.

YALIYOMO

ZLSC Yapata Tunzo ya Asasi Bora, Uk 3


Maalim Seif Awataka Wazanzibari Kutoa Maoni Kuhusu Katiba Mpya, Uk 5

Dhana ya Maslahi Bora ya Mtoto, Uk 8

Tamko la ZLSC Kuhusiana na Fujo Zanzibar, Uk 18

SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi



Toleo Na. 010

Jarida la kila miezi mitatu

Machi - Juni, 2012

Amwagiwa Tindi Kali na Achomewa Moto Nyumba Pemba

TAFITI mbali mbali zimeonesha asilimia 70 ya uvunjifu wa haki za binadamu unafanywa na watu na asilimia 30 tu inazihusisha taasisi za Serikali. Habari hii ni uthibitisho wa uvunjifu wa haki za binadamu unaofanywa na watu. **Polisi** inachunguza tuhuma za kumwagiwa tindi kali (*acid*) Nassor Salim Salahi mkaazi wa Pujini Dodo, Wilaya Chake Chake, Mkoa wa Kusini Pemba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, Bwana Hassan Nasser alithibitisha kupata taarifa za kumwagiwa tindi kali Salahi na alisema wanachunguza waliofanya uhalifu huo.



Bwana Nassor Salim Salahi akiingiza majeraha baada ya kumwagiwa tindi kali (*acid*) huko Pujini Dodo Chake chake, Pemba.

Inaendelea Uk. 19

Tumieni Mahkama Kudai Haki Zinazovunjwa – Jaji Mwampashi

WANANCHI wamesisitizwa kutumia Mahkama kudai haki zao zinazovunjwa badala kulalamika mitaani au kutumia njia zilizo kinyume na sheria.

Wito huo umetolewa na Jaji wa Mahkama Kuu Zanzibar, Mheshimiwa Abraham Mwampashi alipokuwa akizindua Ripoti



Jaji wa Mahkama Kuu Zanzibar, Mheshimiwa Abraham Mwampashi akionesha Ripoti ya Haki za Binadamu ya 2011 muda mfupi baada ya kuizindua katika Ukumbi wa Hoteli ya Bwawani, Zanzibar.

ya Haki za Binadamu ya mwaka 2011 katika ukumbi wa hoteli ya Bwawani.

Jaji Mwampashi alisema kwamba muamko ni mdogo kwa watu wa Zanzibar kutumia Mahkama kudai haki zao zinapovunjwa.

Alisema kwamba inaonekana kuwepo pengo kubwa la ufahamu wa umuhimu wa nafasi ya Mahkama hususan kwa wananchi wa kawaida.

“Ninaishauri taasisi ya ZLSC na taasisi nyengine zinazosimamia haki za binadamu kusimama kidete kutoe elimu ya haki za binadamu,” alisema Jaji Mwampashi.

Matendo mengi yanayosababisha makosa ya ukiukwaji wa haki za binadamu yanaweza kuepukwa ikiwa wananchi watakuwa na elimu tosha ya kuheshimu haki za binadamu.

Alisisitiza kwamba haki za binadamu zinaanza pale binadamu anapozaliwa, ni haki za urithi wala hazitolewi na katiba au sheria yeyote.

Alisema kazi kubwa ya sheria ni kuzitambua, kuzilinda na kuzitekeleza tu haki za binadamu.

Inaendelea Uk. 19